# KUWA SHUJAA WA KIHARUSI!



## JE, KIHARUSI NI NINI?

Kiharusi hutokea wakati damu (na oksijeni) haziwezi kufika ubongoni kwa sababu ya mgando wa damu au mshipa wa damu kukatika.

## BE FAST

### FAHAMU DALILI ZA GHAFLA ZA KIHARUSI

- **B** — **B**ALANCE (KUTOYUMBA): Kuyumbayumba au kizunguzungu
- **E** — **E**YE (JICHO): Hali ya kuona (Jicho) inabadilika
- **F** — **F**ACE (USO): Uso kunyong`onyea
- **A** — **A**RM (MKONO): Mkono kuwa dhaifu au kufa ganzi
- **S** — **S**PEECH (MATAMSHI): Kuwa na matamshi ya kukokoteza
- **T** — **T**IME (WAKATI): Wakati wa kupigia 9-1-1

## TIBA YA HARAKA = UHARIBIFU MDOGO KWENYE UBONGO

- **Pigia 9-1-1** kwa tiba ya haraka au umpeleke mgonjwa wa kiharusi kwenye hospitali haraka iwezekanavyo
- **Kiharusi kinatibika** na kadri mtu anapopata tiba haraka hospitalini, ndivyo kulivyo na uwezekano mdogo wa kuaga dunia au kuwa na ulemavu (kama vile kutoweza kutembea au kuzungumza), kutokana na kiharusi.

### AMRI YA SAUTI

Sema:

- OK Google, call 911 (Sawa Google, pigia 911)
- Hey Siri, call 911 (Hujambo Siri, pigia 911)

### SIMU IMEFUNGWA

- Telezesha juu au gusa kitufe cha Mwanzo
- Gusa Dharura
- Bonyeza 911

BE FAST imetolewa Intermountain Healthcare. BE FAST iliundwa na Intermountain Healthcare, kama mabadiliko ya utekelezaji wa muundo wa FAST na American Stroke Association. Ilitolewa tena kwa ruhusa kutoka Intermountain Healthcare. Hakimiliki 2011, Intermountain Healthcare.

Kansas Department of Health and Environment

KANSAS INITIATIVE FOR STROKE SURVIVAL INC
A Project By & For Kansans